

HALMASHAURI YA WILAYA YA SENGEREMA



Kumb. Na.AB.16/194/02/124,

Tarehe: 29 Machi 2018.

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Kwa mujibu wa kibali cha Ajira Kumb. Na. CFC 26/205/01'FF'/91 cha tarehe 22 Agosti 2017 kama kilivyoongezewa muda kwa kibali Kumb. Na. CFC.26/205/01"GG"/95 cha tarehe 12 Machi, 2018 kutoka kwa Katibu Mkuu (UTUMISHI) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema anawatangazia nafasi za kazi Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi zifuatazo:-

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III NAFASI - 28

SIFA:

Mwenye Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti "Technician Certificate" katika moja ya fani zifuatazo:-

Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

MAJUKUMU YA AFISA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III

- I. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- II. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
- III. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- IV. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- V. Kutafsiri na kusimamia sera Sheria na Taratibu
- VI. Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.


- VII. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalam katika kijiji.
- VIII. Kusimamia kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za vijiji.
- IX. Kutekeleza shughuli nyingine atakazopangiwa na Mwajiri.

NGAZI YA MSHAHARA

Mshahara ni kwa mujibu wa viwango vya mshahara Serikali yaani **TGS B (390,000 X 11,000 hadi 489,000)** kwa mwezi. Mwajiriwa katika kada hii ataanza na mshahara wa shilingi za kitanzania **390,000/=** kwa mwezi.

MASHARTI YA JUMLA

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.
2. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
3. Maombi yote, waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (detailed C.V)
4. Maombi yote ya waombaji yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu (IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (passport size) na iandikwe jina nyuma
5. Testimonials "provisional results" "statement of results" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (**FORM FOUR AND FORM SIX RESULT SLIPS**) **HAVITAKUBALIWA.**
6. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU na NECTA) na taarifa ya uhakiki iambatanishwe kwenye maombi.
7. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
8. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
9. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **18 Aprili 2018 saa 9:30 alasiri**
10. Maombi yote yatumwe kwa:-
Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema,
S.L.P.175,
SENGEREMA.


Magesa M. Boniface
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
SENGEREM

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
S. L. P. 175
SENGEREMA